**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

**MALALAMIKO NAMBA. QN.71/135/110**

**KUDRA PAMBIRE ..............................................................MLALAMIKAJI**

**SHIRIKA LA UGAVI WA UMEME**
**TANZANIA (TANESCO)...................................................MLALAMIKIWA**

---

**TUZO**

---

***(Imetolewa na Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA kupitia kikao chake cha 166 kilichofanyika tarehe 29 Julai, 2021)***

## 1.0 Maelezo ya Awali

Mnamo tarehe 26 Februari 2021, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji "EWURA" ("Mamlaka") ilipokea malalamiko kutoka kwa Bwana Kudra Pambire wa S.L.P 3011, Arusha dhidi ya Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania ("TANESCO") ("Mlalamikiwa"). Mlalamikaji anapinga deni la shilingi 5,064,744.48 ("deni bishaniwa") lililowekwa katika akaunti yake ya LUKU yenye usajili namba 04202946358. Mlalamikaji anadai kwamba alikuwa akimiliki nyumba mbili katika Kata ya Njoro, Manispaa ya Moshi na mnamo tarehe 7 Septemba 2006 aliuza nyumba moja yenye namba H.32/16/NJ kwa ndugu Msafiri Ismael.

Mlalamikaji anadai kwamba nyumba hiyo haikuwa na aina yoyote ya deni dhidi ya mtu yoyote au Mlalamikiwa na kwamba mnunuzi alijiridhisha na hilo kabla ya kusaini mkataba wa mauziano. Kwamba mnamo mwaka 2019, baada ya miaka kumi na tatu, Mlalamikiwa aliibuka na hoja kwamba anamdai Mlalamikaji kiasi cha shilingi 5,064,744.78 kama malimbikizo katika Ankara ya huduma ya umeme.

Mlalamikaji anadai kwamba aliwasilisha nyaraka zote za mauziano kwa Mlalamikiwa ikionyesha kwamba tangu mwaka 2006, umiliki wa nyumba hiyo ulihama kutoka kwake na kwenda kwa Bw. Ismael Msafiri. Mlalamikaji anaeleza zaidi kuwa Mlalamikiwa, kupitia barua yenye kumbukumbu na. RM/KIL/RFO/REV/02 ya tarehe 28 Februari 2020, alihamisha deni hilo kutoka mita namba 04202946358 yenye jina la Mlalamikaji na kwenda mita namba 37142500562 yenye jina la Msafiri Ismail.

Mlalamikaji anadai kwamba baadae, Mlalamikiwa aliamua kuhamisha deni hilo kutoka kwenye mita ya Bw. Ismail na kuliweka katika mita iliyopo kwenye nyumba ya pili inayomilikiwa na Mlalamikaji ambayo haijauzwa na iliyokuwa na wapangaji na kupelekea wapangaji kuondoka. Aidha, Mlalamikaji anadai kwamba kitendo hicho kilipelekea yeye kushindwa kuendelea na biashara ya upangishaji katika nyumba hiyo mpaka leo.

Baada ya kupokea malalamiko ya Mlalamikaji, Mamlaka mnamo tarehe 1 Machi 2021, ilimwandikia Mlalamikiwa na kumuamuru kuleta waraka wa utetezi ndani ya siku ishirini na moja (21) kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (1) cha Kanuni za EWURA za Taratibu za Kutatua Migogoro '*Rule 6 (1) of the Energy and Water Utilities Regulatory Authority (Consumer Complaints Settlement Procedure) Rules, GN No. 428/2020.* Mnamo tarehe 29 Machi 2021, Mlalamikiwa alileta utetezi wake na kuiambia Mamlaka kwamba chanzo cha malalamiko ni deni la shilingi 5,064,744.78 ambalo ni malimbikizo ya matumizi ya umeme kwa kipindi cha nyuma katika moja ya nyumba ya Mlalamikaji iliyoko Kata ya Njoro, Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro. Deni tajwa liliwekwa katika mita namba 04202946358 kwa jina la Kudra Pambire.

Mlalamikiwa alieleza kwamba baada ya kufanya uchunguzi kuhusiana na malalamiko ya Mlalamikaji, walibaini kwamba nyumba iliyouzwa mnamo tarehe 7 Septemba 2006 haikuwa na miundombinu ya umeme yaani iliuzwa bila mita ya umeme. Pia mnunuaji wa nyumba hiyo Bwana Msafiri Ismael alikiri kuuziwa nyumba hiyo bila miundombinu yoyote ya umeme na baadae kuunganishiwa umeme kwa mita ya zamani kama ilivyokuwa utaratibu wa Mlalamikiwa. Mlalamikiwa alieleza kuwa walibadilisha mita hiyo na kuweka mita ya LUKU

yenye namba 3742500562 kwa jina la Msafiri Ismail kwa mantiki hiyo, deni hilo halimhusu Bw. Ismail kwani alifanya maombi upya ya huduma ya umeme kwa jina lake. Mlalamikiwa alieleza kwamba, mnamo tarehe 24 Aprili 2020, alilazimika kutafuta akaunti nyingine ya Mlalamikaji na kuweka deni la kiasi cha shilingi 5,064,744.78 ikiwa ni malimbikizo ya matumizi ya umeme katika nyumba aliyouza kwa Bwana Ismail.

Juhudi za kutafuta suluhu zilifanywa chini ya uagalizi wa kitengo cha Malalamiko cha Mamlaka lakini muafaka haukuweza kufikiwa. Kwa sababu hiyo, malalamiko yalipelekwa mbele ya Divisheni ya Mamlaka kwa ajili ya usikilizwaji.

## 2.0 <u>Usikilizwaji wa Shauri</u>

Mnano tarehe 20 Mei 2021, malalamiko haya yalikuja kwa ajili ya kusikilizwa na Mlalamikaji aliwakilishwa na Bwana Alexander Peter, Wakili Msomi na Mlalamikiwa aliwakilishwa na Bwana Karonda Kibamba, Afisa Sheria Mkuu wa Mlalamikiwa. Wakati wa usikilizwaji wa shauri, hoja zilizobishaniwa zilikuwa zifuatazo:

1) *je deni la shilingi 5,064,744.78 ni la Mlalamikaji;*
2) *je Mlalamikaji anapaswa kumlipa Mlalamikiwa deni la shilingi 5,064,744.78 ;*
3) *nafuu gani pande zote zinastahili?*

Wakati ya usikilizwaji wa shauri, Mlalamikaji alikuwa na mashahidi watatu ambao ni Mariam Kudra, shahidi wa kwanza (CW1), Bwana Oswald Kimbi shahidi wa pili (CW2) na Bwana Nemes Joseph Kimario, shahidi wa tatu (CW3). Katika utetezi wake CW1 alitoa nakala ya mkataba wa mauziano ya nyumba wa tarehe 7 Septemba 2006 kama ushahidi uliopokelewa kama kielelezo «C1 », barua ya kwenda kwa Mlalamikiwa ya tarehe 10 Disemba 2019 ambayo ilipokelewa kama kielelezo « C2 » na barua ya tarehe 8 Februari 2020 iliyopokelewa kama kielelezo « C3 ». Kwa upande mwingine, Mlalamikiwa alikuwa na shahidi mmoja ambae ni Bw. Robson J. Chaya ambaye ni Mhasibu

wa Mlalamikiwa (RW). RW alitoa nakala ya Taarifa za Akaunti ya Matumizi ya Umeme ya Mlalamikaji kutoka mfumo wa *Custima* na *HiAffinity* pamoja na Taarifa ya Akaunti ya Matumizi ya Umeme ya Msafiri Ismael ambavyo vilipokelewa kama vielelezo "R1" hadi "R6".

## 3.0 Uamuzi:

Katika hatua za kufikia uamuzi, Mamlaka imezingatia sheria mbalimbali ikiwa ni pamoja na Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, Sheria ya Umeme, Sura ya 131 ya Sheria za Tanzania na Kanuni za EWURA za Taratibu za Kutatua Migogoro Tangazo la Serikali Na. 428 la 2020 *(EWURA (Consumer Complaints Settlement Procedure) Rules GN. No. 428/2020)* na Kanuni za Huduma za Uuzaji Umeme Tangazo la Serikali Na. 387 la 2019 *(Electricity (Supply and Services) Rules GN.No. 387/2019.* Mamlaka pia imezingatia ushahidi wa maneno na wa maandishi uliotolewa na mashahidi wakati wa usikilizwaji shauri. Maamuzi ya hoja zinazobishaniwa ni kama ifuatavyo :

**Hoja Na. 1 : Je deni la shilingi 5,064,744.78 ni la Mlalamikaji ?**

Kwenye kujibu hoja hii, tumepitia ushahidi wa maneno, maandishi pamoja na mashahidi wa Mlalamikaji na Mlalamikiwa. CW1 alieleza kwamba yeye na mume wake walikuwa na nyumba ambayo walimuuzia Bwana Msafiri Ismael mnamo tarehe 7 Septemba 2006. CW1 alieleza kwamba yeye ndio aliyesimamia zoezi zima la uuzwaji wa nyumba hiyo na kwamba pande zote mbili ziliandikishana mkataba ambao ulipokelewa kama kielelezo « C1 » na baada ya siku kadhaa Bwana Ismail alirudi kwa CW1 na kuomba jalada la matumizi ya umeme na maji ya nyumba husika kwa ajili ya kubadilisha jina la umiliki.

CW1 alikiri kwamba alimtaarifu Mlalamikiwa kwa barua kuhusu uuzwaji wa nyumba hiyo, mwaka 2019, pale ambapo deni lilihamishwa kutoka nyumba iliyouzwa na kupelekwa kwenye nyumba nyingine ya Mlalamikaji. CW1 alitoa barua hiyo kama kielelezo « C2 ». CW1 aliendelea kueleza kwamba baada ya

kuandika barua hiyo, Mlalamikiwa alihamisha deni hilo na kulipeleka kwenye nyumba ya Msafiri Ismail na kumwandikia barua ambayo aliitoa kama kielelezo « C3 » ambapo alimfahamisha kwamba baada ya kujiridhisha, amehamisha deni hilo kutoka mita namba 04202946358 yenye jina la Kudra Pambire, na kwenda mita namba 37142500562 yenye jina la Msafiri Ismail kama alivyoomba. CW1 alieleza kwamba baada ya mwezi mmoja, deni hilo lilirejeshwa tena kwenye mita yake na akaanza kukatwa asilimia hamsini ya manunuzi yake ya umeme na kwamba makato hayo yanaendelea mpaka leo.

Wakati wa maswali ya dodoso, wakili wa Mlalamikiwa alimuuliza CW1 kama wakati anamuuzia nyumba Bwana Ismail, alimtaarifu Mlalamikiwa ambapo alijibu hapana. CW1 aliulizwa kuwa wakati wa uuzwaji wa nyumba kama kulikuwa na deni ambapo alijibu ndio. Alipoulizwa tena juu ya kiasi cha deni hilo, alisema hakumbuki. Wakili wa Mlalamikiwa alimuuliza tena kama wakati anamkabidhi Bwana Ismail jalada la maswala ya umeme, je alimuonyesha deni lilikuwa ni kiasi gani na ni kiasi gani kilikuwa kimeshalipwa, CW1 alisema hakumbuki.

Wakili wa Mlalamikiwa aliendelea kumuuliza CW1 kwamba sababu pekee ya yeye kutohusika na deni ni kwasababu alishauza nyumba hiyo ambapo alijibu ndio. CW1 aliulizwa pia kama anachobishania sio uwepo wa deni bali ni nani anapaswa kulilipa, na akajibu ndio. Alipoulizwa je ni kwanini Bwana Ismail ndiye anapaswa kulipa deni na sio Mlalamikaji, CW1 alidai kwamba Bwana Ismail alipoinunua nyumba hiyo, alikuwa amejiridhisha na maswala yote yanayoihusu nyumba hiyo yakiwemo maswala ya umeme. CW1 aliulizwa kama wakati wa uuzwaji wa nyumba hiyo, kulikuwa na umeme pamoja na miundombinu ya umeme ambapo alijibu ndio.

Alivyoulizwa na mjumbe wa Mamlaka ni jinsi gani Bwana Ismail alijiridhisha na kila kitu kinachohusiana na nyumba hiyo kama anavyodai, CW1 alidai kwamba Bwana Ismael alifanya utafiti katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mamlaka za Maji na Umeme. Kwa kuwa huo ndio utaratibu unaojulikana pale mtu anaponunua nyumba, yeye aliamini kwamba Bwana Ismael atakuwa alifanya utafiti huo.

CW1 aliulizwa na mjumbe wa Mamlaka kama anajua ni taarifa gani zilikuwepo kwenye jalada alilompa Bwana Msafiri, CW1 alidai kwamba alimpatia Bwana Msafiri jalada likiwa na ankara za umeme pamoja na taarifa za akaunti ya umeme ya nyumba hiyo, taarifa za kumuwezesha kubadili jina. Aidha CW1 aliwakabidhi wapangaji waliokuwemo kwenye nyumba hiyo kwa Bwana Ismael kama mmiliki mpya wa nyumba hiyo. CW1 aliongezea kwa kusema kwamba Bwana Ismael alijua kuhusu uwepo wa deni hilo. Alivyoulizwa ni lini alianza kupangisha watu kwenye nyumba hiyo, CW1 alijibu kwamba kuanzia mwaka 1998 na kwamba kabla ya kuwa na wapangaji, alikuwa akiishi katika nyumba hiyo.

CW2 alieleza kwamba Mlalamikaji aliwahi kuishi katika nyumba hiyo katika mtaa wa Viwanda na kwamba aliuza nyumba yake na yeye alikuwepo kama shahidi wakati wa mauziano hayo. Alipoulizwa kama nyumba hiyo imekuwa ikipata huduma ya umeme kwa muda wote, ambapo alijibu ndio. Kwa upande wake, CW3 alieleza kwamba aliwahi kuwa mpangaji mnamo mwaka 2001 katika nyumba iliyouzwa na Mlalamikaji mpaka mwaka 2017 na kwamba alikuwepo kipindi nyumba hiyo inauzwa kwa Bwana Ismael. CW3 alieleza kwamba nyumba hiyo ilikuwa na umeme na wapangaji wote walikuwa wanampa Mlalamikaji fedha ya kulipia umeme kwa ajili ya kulipia huduma hiyo. Aidha, CW3 alieleza kwamba nyumba ilikuwa na wapangaji wanne na yeye alikuwa amepanga sehemu ya nyumba hiyo kama duka akiuza nafaka na vinywaji na alikuwa na jokofu. CW3 alieleza pia kwamba hakukuwahi kuwa na matatizo yoyote ya huduma ya umeme katika nyumba hiyo.

Wakati wa maswali ya dodoso, CW3 alieleza kwamba kati ya mwaka 2001 na Agosti 2006, Mlalamikaji ndio alikuwa analipia umeme na hakuwahi kwenda mwenyewe kulipia umeme. CW3 alieleza kwamba baada ya umiliki kuhama kwa Bwana Ismael, muda mwingine alikuwa analipia umeme mwenyewe. CW3 aliulizwa mita iliyokuwa inatumika kipindi nyumba haijauzwa ilienda wapi, ambapo alijibu hafahamu. CW3 aliulizwa tena na wakili wa Mlalamikiwa kama kipindi Mlalamikiwa anaweka mita kwenye nyumba ya Bwana Ismael, walikuta mita nyingine, CW3 alisema hafahamu kwasababu hakuwepo dukani muda

wote. CW3 alieleza kwamba hakuwahi kumsikia Mlalamikaji akimtaarifu Bwana Ismael kuhusu deni lolote la umeme.

CW3 aliulizwa na Mamlaka kama kuna kipindi chochote kati ya mwaka 2001 na 2017 ambapo hakukuwa na huduma ya umeme katika nyumba hiyo, na alijibu kwamba umeme ulikuwepo siku zote. CW3 alieleza kwamba kwa kipindi chote mita ilikuwa moja tu katika nyumba hiyo ila mwanzoni ilikuwepo mita ya zamani, na baadae ikawekwa mita mpya ya LUKU. CW3 alidai kwamba mita ya zamani ilibadilishwa na siku hiyo hiyo iliwekwa mita ya LUKU kwahiyo hakukuwa na kipindi nyumba ilikuwa bila umeme.

CW3 aliulizwa wakati anaenda kulipia umeme, risiti ilikuwa inatoka kwa jina gani, ambapo alijibu kwamba jina la Bwana Ismael na kwamba malipo aliyafanya mwaka 2008/2009. Aidha, aliulizwa kama Mlalamikiwa alikuwa anadai chochote, akasema hapana. CW3 aliendelea kuelezea kwamba Bwana Ismael aliwaagiza wapangaji wote wawe wanalipia umeme wenyewe badala ya kumpa fedha yeye.

Kwa upande wake, Mlalamikiwa kupitia shahidi wake RW alieleza kwamba mnamo mwaka 2006 wakati nyumba inauzwa, deni lilkuwepo la shilingi 2,291,013.09. RW alieleza kwamba mpaka kufikia tarehe 31 Septemba 2006, deni lilikuwa shilingi 1,853,825.45 baada ya shilingi 437,187.64 kulipwa. RW alieleza kwamba pale ambapo deni halijalipwa kuna kuwa na gharama za huduma pamoja na riba, mpaka pale Mlalamikiwa atakapo sitisha huduma. RW alieleza pia kwamba kuanzia Oktoba 2006 hadi tarehe 26 Aprili 2019, Mlalamikiwa alisitisha gharama za huduma kwenye mifumo yake kwenye akaunti ya Mlalamikaji na katika kipindi hicho kulikuwa na deni la shilingi 3,417,947.33 ikijumuisha riba, gharama za matumizi ya umeme pamoja na gharama za huduma.

Mnamo tarehe 26 Aprili 2019 deni lilikuwa shilingi 5,271,772.78 na siku hiyo hiyo RW alidai kwamba deni lilihamishwa kutoka kwenye mita ya zamani na kuwekwa kwenye mita ya LUKU ya Mnunuzi Bwana Ismael na tarehe 2 Mei 2019 likaingizwa kwenye mita namba 04202946358 iliyopo kwenye nyumba ya

Mlalamikaji. Wakati deni linahamishwa, lilikuwa limepunguwa na kufikia shilingi 5,064,744.78 baada ya makato kwa njia ya LUKU.

Aidha, RW alieleza kwamba mpaka tarehe 20 Mei 2021 makato katika akaunti hiyo yalikuwa shilingi 418,371.00 deni likibakia kuwa shilingi 4,853,401.78 ambapo deni halisi likiwa shilingi 1,836,704 na riba ya shilingi 3,016,697.47. RW alieleza kwamba Mlalamikaji ndiye anaedaiwa deni hilo kwasababu yeye ndiye aliyetumia umeme huo kwenye mita hiyo mpaka mwezi Septemba 2006 na sio Bwana Ismail. RW alieleza kwamba hakukuwa na uthibitisho wa vigezo na masharti ya uuzwaji wa nyumba hiyo kwamba atakayenunua nyumba hiyo, atawajibika kulipia deni hilo la Mlalamikaji. RW alieleza kwamba Mlalamikiwa alikuwa tayari kufuta riba endapo Mlalamikaji angekubali kulipa deni halisi kwasababu ni deni la muda mrefu.

RW aliwakilisha vielelezo R1, R3, R4 ambavyo vilionyesha matumizi ya umeme kwenye mita namba 73015312 yenye jina la Kudra Pambire kuanzia mwaka 2000 mpaka mwaka 2019. Pia kielelezo « R2 » kikionyesha matumizi ya umeme kipindi ambacho Bwana Ismail aliweka mita yake ya zamani kwenye nyumba aliyonunua akiwa na mita ya zamani namba 73059503. Kielelezo « R5 » kilitolewa kuonyesha uhamishwaji wa deni kwenda kwa Mlalamikaji na deni linalosalia baada ya makato ya LUKU. Katika kumalizia, RW alitoa kielelezo « R6 » kuondolewa kwa deni hilo kwenye akaunti ya Bwana Ismail.

Wakati wa maswali ya dodoso, Mlalamikaji alimuuliza RW kama nyumba hiyo iliuzwa bila mita ambapo alijibu ndio. RW alieleza pia kwamba baada tu ya kununua nyumba hiyo, Bwana Ismail aliweka mita yake ya zamani kwahiyo hakutumia kabisa mita ya Mlalamikaji. RW alieleza kwamba Mlalamikaji alipewa ankara ya mwisho ya umeme mwezi Oktoba 2006. RW alieleza kwamba walipochunguza ankara za umeme, walibaini kwamba zilikuwa za Septemba 2006 na kwamba Bwana Ismail hakuwahi kutumia mita ya Mlalamikaji.

RW alieleza kwamba, wakati Bwana Ismail ananunua nyumba hiyo, hakukuwa na mita na kwamba mita iliyokuwa inatumika, haikuwahi kuonekana. RW alidai

kwamba yawezekana Bwana Ismail alibaini kwamba nyumba ina deni na kuamua kutumia mita yake na sio aliyoikuta. Alivyoulizwa na Mamlaka kama walijua kama mita ya Mlalamikaji ina deni, RW alieleza kwamba kipindi hicho hakukuwa na mawasiliano mazuri kati ya mafundi na wahasibu na kwamba ilichukua muda mrefu kuhamisha deni kwasababu ya walakini katika mifumo yao ya ndani. RW alieleza kwamba mnamo tarehe 29 Agosti 2018, ndio waliweza kuthibitisha madeni kwenye vitabu na kwenye eneo nyumba ilipo.

Tumepitia ushahidi wote wa maneno na maandishi ulioletwa na pande zote mbili na tunashukuru kwa ushahidi huo. Sheria inamtaka anayedai kuthibitisha madai yake kwa hivyo Mlalamikaji anapaswa kuthibitisha kwamba ni kweli hilo deni linalobishaniwa sio la kwake bali ni la Bwana Ismail. Hoja kuu iliyoelezwa na Mlalamikaji ni kwamba Bwana Ismail anapaswa kulipa deni lililowekwa kwenye mita ya Mlalamikaji na Mlalamikaji habishi kwamba kulikuwa na deni bali kwamba yeye hastahili kulilipa kwasababu wakati Bwana Ismail ananunua nyumba, alijiridhisha na kila kitu kuhusiana na nyumba hiyo. Kwa maneno yake mwenyewe, CW1 alikiri uwepo wa deni kabla ya nyumba kuuzwa na kielelezo « R1 » kipo wazi kabisa kwamba asili ya deni ni la Mlalamikaji kwasababu deni hilo limeanza malimbikizo mwaka 2000 mpaka tarehe 31 Septemba 2006 ambapo Mlalamikaji bado alikuwa anamiliki nyumba hiyo. Kwa kuwa wapangaji ndio waliokuwa wanampa Mlalamikaji fedha kwa ajili ya kulipia umeme, hii inaashiria kwamba Mlalamikaji hakuwa anafanya malipo yoyote au malipo kamili ya umeme kulingana na matumizi.

Aidha, kuna utata juu ya upotevu wa mita ya zamani ya Mlalamikaji kwa sababu wakati Bwana Ismail anaweka mita yake, hakukuwa na mita nyingine katika nyumba hiyo na haijulikani hiyo mita imeenda wapi. CW1 alidai kwamba miundombinu yote ikiwemo mita ilikuwepo wakati Bwana Ismail ananunua nyumba ila RW amekanusha kwamba wakati Bwana Ismail anawekewa mita, hakukuwa na mita nyingine katika nyumba hiyo.

Kuanzia tarehe 1 Oktoba 2006, mita iliyotumika katika nyumba husika, ilikuwa ya Bwana Ismail kwa hiyo hakuna mtu mwingine yeyote aliyetumia mita ya Mlalamikaji, zaidi ya Mlalamikaji mwenyewe. Hivyo basi, tumejiridhisha

kwamba umeme ulitumika kabla ya nyumba kuuzwa na hivyo basi deni bishaniwa kiasi cha TZS 5,064,744.78 ni deni dhidi ya Mlalamikaji.

**Hoja Na. 2: Je, Mlalamikaji anapaswa kumlipa Mlalamikiwa deni la shilingi 5,064,744.78 ;**

Kwa kuwa jibu la hoja ya kwanza ni kwamba deni ni la Mlalamikaji, basi anapaswa kumlipa Mlalamikiwa deni hilo la shilingi 5,064,744.78. Lakini pamoja na hayo, mwenendo wa Mlalamikiwa, unaonyesha kutokufuatiliwa kwa deni ambalo limelimbikizwa tangu mwaka 2000 na deni likihamishwa kutoka kwenye mfumo wa *Custima* hadi mfumo wa *HiAffinity*. Mlalamikiwa alikiri kuchelewa kudai deni hilo kutoka kwa mteja wake Bw. Pambire na kutokufahamu uelekeo wa mita iliyokuwa inatumiwa na Mlalamikaji. Katika hali ya kawaida haikupaswa kumchukua Mlalamikiwa miaka kumi na tatu kudai deni hilo. Kutokana na kwamba Mlalamikiwa alichelewa kudai deni, ni maoni yetu kwamba alishindwa kutimiza wajibu wake kisheria kumdai Mlalamikaji deni na kutokuchukua hatua stahiki kipindi hicho cha nyuma.

Kwa mujibu ya Kanuni 48(1)(b) ya Kanuni za Uuzaji Umeme kwa wateja wa mwisho Tangazo la Serikali Namba 387/2019 *(the Electricity (Supply Services) Rules, GN. No.387 of 2019)*, inasema kwamba Mlalamikiwa ana jukumu la kukagua na kupima mita ya mteja yoyote ili kuangalia umeme unaotumika angalau mara moja kila baada ya miezi ishirini na nne kwa wateja wa kawaida. Kanuni hii inasema kama ifuatavyo na tunanukuu kwa lugha ya Kiingereza :

> *48 (1)"A licensee shall inspect and test a meter of any customer in order to verify amount of electrical energy consumed at least once in every:*
> *(b) twenty-four months for other customers."*

Kwa kuwa Mlalamikiwa ndiye mtoa huduma pekee wa nishati ya umeme nchini na mita zote ziko chini ya uangalizi wake, yeye ana jukumu la kukagua mita zote za wateja na kuchukua hatua zinazostahili pale ambapo changamoto inajitokeza. Aidha, Mlalamikiwa alipaswa kujua kama nyumba husika ilishawahi kuwa na umeme na kwamba ina deni kabla ya kumfungia umeme Bwana

Ismail. Maelezo ya RW kwamba hakukuwa na mawasiliano mazuri kati ya wahasibu na mafundi hayana mashiko kwa kuwa mawasiliano duni kati ya maafisa wa Mlalamikiwa hayawezi kuwa kigezo cha Mlalamikiwa kutotimiza wajibu wake na ni kielelezo cha mapungufu kwa upande wao. Inaonekana kwamba Mlalamikiwa alichelewa kudai deni kwa muda kwa kuwa hakuwa na uhakika juu ya mdeni wake. Mlalamikiwa angetimiza wajibu wake huu mapema, Mlalamikaji angelazimika kulipa deni hilo kwa mujibu wa sheria.

Ni mtazamo wetu kwamba Mlalamikiwa katika suala hili, hakuwajibika ipasavyo kwa kuwa alishindwa kukusanya deni hili mapema na kwa mdaiwa sahihi. Aidha, mojawapo ya misingi ya utoaji wa haki ni muda, kwamba madai yoyote ili yaweze kusikilizwa na kupewa nafuu, lazima yaletwe ndani ya muda stahiki. Msingi huu wa kisheria umetokana na ukweli kwamba ni katika maslahi ya umma, kuwapo na ukomo wa madai. Aidha, madai yanapoletwa ndani ya muda inasaidia kwenye kutenda haki kwani muda ukipita sana, kumbukumbu na ushahidi hupotea. Sheria ya Umeme, Sura ya 131 ya Sheria za Tanzania pamoja na Kanuni za Umeme, Tangazo la Serikali Na. 63 la 2011 *(Electricity (General) Regulations, GN No. 63/2011* na Kanuni za Huduma za Umeme, Tangazo la Serikali Na. 387 la 2019 *(Electricity (Supply Services) Rules, GN No. 387/2019*, ziko kimya kwenye suala zima la muda ambao Mlalamikiwa anaweza kudai madeni yake.

Hata hivyo, kwa kuwa uhusiano wa Mlalamikaji na Mlalamikiwa ni wa kimkataba, na kutokana na kukosekana kwa uwepo wa ukomo wa kuleta madai kwenye sheria tajwa hapo juu, tumelazimika kukopa kwenye Sheria mama ya Ukomo wa Madai, Sura ya 89 ya Sheria za Tanzania *(Law of Limitation Act, Cap. 89)* ambayo imeweka ukomo wa madai yatokanayo na mikataba kuwa miaka sita. Kumbukumbu zinaonesha kwamba deni bishaniwa ni la muda mrefu sana tokea mwaka 2000, yaani miaka 21 iliyopita. Kwa kuzingatia sheria tajwa hapo juu ni dhahiri kuwa madai yoyote kuhusiana na deni bishaniwa yako nje ya muda.

Hivyo basi, na kwa kuzingatia uchambuzi wetu hapo juu ni dhahiri kwamba deni linapaswa kulipwa na Mlalamikaji lakini limepitwa na ukomo wa muda wake wa

kudaiwa kwa mujibu wa sheria na kwa msingi huo, Mlalamikaji hastahili kulipa deni hilo.

**Hoja Na. 3: Je, nafuu gani pande zote zinastahili ?**

Kwenye malalamiko haya, Mlalamikaji anaomba Mlalamikiwa aagizwe yafuatayo:

a) kufuta deni lote la shilingi 5,064,744.78 kwa Mlalamikaji lililotokana na mita inayobishaniwa;
b) kulipa gharama za usumbufu ; na
c) kulipa nafuu zozote Mamlaka itakazoona zinafaa.

Kwa upande mwingine, Mlalamikiwa anaomba malalamiko haya yatupiliwe mbali na Mlalamikaji aagizwe kulipa deni. Kutokana na ushahidi uliotolewa pamoja na jibu letu kwenye hoja ya kwanza na ya pili, Mlalamikiwa anaagizwa kama ifuatavyo :

a) kufuta deni lote la shilingi 5,064,744.78 kwa Mlalamikaji lililotokana na mita inayobishaniwa; na
b) kurejesha kiasi chote cha fedha ambazo zimekatwa kulipia deni husika hadi sasa.

Kulingana na aina ya malalamiko haya na ushiriki wa kila upande katika malalamiko haya tunaagiza kila upande ugharamie gharama za kuendesha malalamiko haya.

**IMETOLEWA KWA LAKIRI** ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji Dodoma tarehe 29 Julai, 2021.

..............................

**KAPWETE LEAH JOHN**
**KATIBU WA BODI**